*Kanisa la Waadventista Wasabato – Jimbo la Mara*

**SHULE YA SEKONDARI IKIZU**

S.L.P. 245, MUSOMA-TANZANIA

**Ofisi ya Mkuu wa Shule**

*simu:+255784288440/0765434991* *Barua Pepe: ikizuhigh@gmail.com*

*Tovuti: www.ikizuhighschool.ac.tz*

Mpendwa, ______________________________________________September, 2021._

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA IKIZU KATIKA KIDATO CHA KWANZA 2022.

Napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako kuingia kidato cha KWANZA hapa Ikizu mwaka 2022. Tunaamini kuwa huu ni mpango wa Mungu kwako kupata moja ya nafasi adimu ya kuendelea na masomo ya Sekondari hapa Ikizu. Unaombwa kuitumia kwa busara, sala, nidhamu na bidii kubwa nafasi hii ili gharama kubwa za kukusomesha zilete manufaa makubwa kwako, kwa Ndugu zako na kwa Taifa letu zuri la Tanzania. Mungu akubariki wewe na wote ambao kwa hali na mali watajitolea kufanikisha kisomo chako hapa Ikizu.

### A. AINA YA SHULE:

Shule hii inamilikiwa na kuendeshwa na Kanisa la Waadventista Wasabato. Ilianzishwa mwaka 1912 na Wamisionari toka Ujerumani. Hivi sasa inatoa elimu ya kidato cha kwanza hadi cha sita kwa wavulana na wasichana.

### B. MIONGOZO:

Shule hii hutumia miongozo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Elimu ya juu Tanzania pamoja na sera ya Elimu ya Kanisa la Waadventista Wasabato ulimwenguni. Hii ni pamoja na kuhudhuria ibada zote zinazoendeshwa hapa shuleni. Pia unahimizwa kuzitunza **AMRI zote KUMI ZA MUNGU** ikiwemo amri ya utunzaji wa **SABATO YA BWANA MUNGU (Jumamosi) soma Kutoka 20:1-11.**

### C. SHERIA ZA SHULE

NB: Lugha ya mawasiliano na kufundishia ni Kiingereza.

Sheria na taratibu zote za shule hii kwa kufuata miongozo iliyopo katika **STUDENT'S HANDBOOK.** Kijitabu hicho ni lazima upewe mara tu uingiapo shuleni.

Yafuatayo ni makosa yatakayosababisha mwanafunzi kuchukuliwa hatua za nidhamu, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule mara moja. Mzazi zingatia

1. Kupiga au kupigana.
2. Kumgomea mwalimu au mfanyakazi wa shule.
3. Ulevi wa pombe, uvutaji sigara au madawa ya kulevya ama kupatikana na vitu hivyo.
4. Wizi wowote ama uharibifu wa mali ya shule kwa makusudi.
5. Uasherati.
6. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule.
7. Kukwepa masomo au mitihani na kutohudhuria vipindi bila ruhusa ya mwalimu wa somo au wa zamu.
8. Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni.
9. Kudharau, kukwepa au kukashifu ibada zinazoendeshwa shuleni.
10. Kwenda kwenye nyumba za watumishi **bila ruhusa ya mkuu wa shule** ni marufuku.
11. Kuchelewa shule bila sababu za msingi.
12. Kumiliki Simu, Radio, Camera kisu, panga na vitu vyote vya aina hiyo.

NB: Simu ni haramu kituoni hapa ukionekana au kugundulika unamiliki simu **utafukuzwa shule mara moja (ZINGATIA)**.

## D. KUJA SHULE

Unatakiwa kuja shuleni tarehe **05/01/2022 (Jumatano)** Endapo utakuwa hujaripoti shuleni ifikapo tarehe 17/01/2022 nafasi yako itagawiwa kwa mwingine na wewe hautapokelewa hata kama utakuwa umesafiri safari ndefu na umejiandaa vema. Tafadhali tujulishe kwa simu iwapo unazo sababu muhimu za kuchelewa ili tuitunze nafasi yako. Fanya mawasiliano hayo kwa namba ya Mkuu wa Shule au Makamu wa Mkuu wa Shule tu. Na. za simu zinaonyeshwa ukurasa wa 6. **Usije siku ya Sabato (Jumamosi)** au Jumapili. Mwisho wa kuripoti ni saa 11:00 jioni.

Shule hii iko katika kijiji cha Bukama, kata ya Nyamuswa, wilaya ya Bunda mkoa wa Mara. Unaweza kufika shuleni kwa kusafiri njia zifuatazo:

| | | |
|---|---|---|
| Bunda | - | Nyamuswa (nauli Sh. 2,500=) |
| Musoma | - | Nyamuswa (nauli Sh. 4,000=) magari madogo madogo |
| Bunda | - | Misheni/ Bukama (basi – nauli sh. 4,000=) |
| Nyamuswa | - | Ikizu Sekondari/Mission nauli 1,500/= kwa pikipiki |
| Mugumu/Serengeti | - | Bukama (Basi – Nauli sh. 6,000=) |

Kutoka Nyamuswa hadi hapa shuleni ni mwendo wa saa moja kwa kutembea. Si salama kutembea usiku. Ni bora kukodi gari ndogo Nyamuswa shs. 5,000= (Elfu tano tu) au pikipiki ambayo ni shs. 1,500= (Elfu moja mia tano tu) ikiwezekana kwa kusaidiana na abiria wengine hasa wanafunzi hadi shuleni.

## E. KUANZA MASOMO.

Shule hii itajitahidi kukujengea mazingira mazuri ya kusoma na kufaulu. Wahi uanze pamoja na wenzako. Mwisho wa mwaka utatakiwa kuwa na wastani wa asilimia zisizopungua **45%** ya masomo yako. Ukishindwa hautaruhusiwa kwenda kidato kingine badala yake utatakiwa kurudia darasa kwa gharama zingine tena. Hivyo wazazi hawakuleti kucheza bali kufanya kazi kwa bidii zote. Usiwakatishe tamaa wazazi wako kwa uvivu au utovu wa nidhamu bali tumia juhudi, maarifa na sala.

Sambamba na masomo ni LAZIMA kushiriki shughuli zote za kilimo, usafi wa mazingira na mabweni, pamoja na MICHEZO. Ni wale tu wenye matatizo makubwa ya kiafya, **wenye vyeti vya daktari anayetambuliwa na watakaothibitishwa na mganga wa shule hii,** ndio watakaoruhusiwa kufanya shughuli rahisi. Hapa hakuna **mabwana** na **watwana.** Kazi ni wajibu na baraka kwa wote.

## F. ADA, MICHANGO NA MAHITAJI MENGINE

(tumeambatanisha katika fomu hii ukurasa wa 3) **ANGALIA na KUZINGATIA** endapo utakuwa na uhitaji wa ufafanuzi wasiliana nasi kwa namba **0757-141119 au 0621-074521.**

# KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO
# JIMBO LA MARA
## SHULE YA SEKONDARI IKIZU

**NMB Bank A/C** **30302300966**

**NBC Bank A/C** **030103000830**

**TCB Bank A/C** **380227000006**

Jina la akaunti ni **IKIZU HIGH SCHOOL**

**Andika jina la mwanafunzi na kidato kwenye bank slip siyo jina la aliyelipa.**

### MCHANGANUO WA ADA KWA MWAKA 2022 -BWENI (O-LEVEL)

| KIDATO | MWEZI JANUARY | MWEZI APRIL | MWEZI JULY | MWEZI SEPTEMBER | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| I | 871,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 1,941,400 |
| II | 898,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 1,968,400 |
| III | 848,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 1,918,400 |
| IV | 925,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 1,995,400 |

### MCHANGANUO WA ADA KWA MWAKA 2022 - KUTWA (O-LEVEL)

| KIDATO | MWEZI JANUARY | MWEZI APRIL | MWEZI JULY | MWEZI SEPTEMBER | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| I | 736,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,491,400 |
| II | 763,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,518,400 |
| III | 713,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,468,400 |
| IV | 790,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,545,400 |

### MCHANGANUO WA ADA KWA MWAKA 2022/2023 - BWENI (A-LEVEL)

| KIDATO | MWEZI JULY | MWEZI SEPTEMBER | MWEZI JANUARY | MWEZI APRIL | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| V | 838,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 1,908,400 |
| VI | 941,400 | 300,000 | 520,000 | 250,000 | 2,011,400 |

### MCHANGANUO WA ADA KWA MWAKA 2022/2023 - KUTWA (A-LEVEL)

| KIDATO | MWEZI JULY | MWEZI SEPTEMBER | MWEZI JANUARY | MWEZI APRIL | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| V | 703,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,458,400 |
| VI | 806,400 | 210,000 | 380,000 | 165,000 | 1,561,400 |

*Unapoamua kuacha shule au kufukuzwa shule* **HAKUNA KARO WALA SEHEMU YOYOTE YA MALIPO ITAKAYORUDISHWA.**

**NB:** kama mwanao anayo BIMA YA AFYA (NHIF) Aje nayo, ambao hawana shule itashughulikia kwa ajili ya TIBA yake..

Malipo yote ya fedha za shule yafanywe kupitia **Benki tu**. Tafadhali ukifika shuleni usimpatie mtu mwingine fedha yoyote ya malipo isipokuwa Cashier wa shule ambaye lazima akupatie risiti ya malipo uliyofanya kwa muda huo huo.

Watakaokula karo au fedha yoyote waliyopewa na wazazi kwa ajili ya malipo ya shule watachukuliwa hatua za kinidhamu kama sheria za shule zilivyo. **Hii ni pamoja na kufukuzwa shule.** Tafadhali wahurumie wanaokulipia karo uwe mwaminifu na Mungu atabariki kazi yako.

**VIFAA ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO.**

1. **SARE YA SHULE**

***Wasichana:***

- Sketi mbili **Dark blue** zenye marinda (kitambaa cha suti), urefu hadi chini.
- Blauzi 2 nyeupe, mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika mguu vyenye kamba visigino vifupi.
- Soksi ndefu nyeupe (stocking) doti 2
- Nguo za baridi atapewa sweta maalumu lenye nembo ya shule (la kijani) akifika shuleni.
- Truck Suti ya Blue kwa wasichana kwaajili ya michezo.
- Viatu vya wazi vyeusi (open shoes) pair moja kwa kushindia baada ya saa za madarasa **(visiwe yeboyebo).**
- Nguo ya kulalia (night dress) nyepesi.
- Suti nyeusi pande nane kwa ajili ya uniform ya kanisani **(inchi 10)** kutoka kwenye goti kwenda chini, koti lenye mikono mirefu lenye vishikizo viwili hadi vitatu na liwe na kola
- Shati la light blue lenye mikono mirefu la kuvalia suti siku ya ibada (Jumamosi).
- Kanda mbili za bafuni.

**NB: Nywele ndefu, kusuka nywele, curl, rangi za mdomo na kucha, wanja, bangili, heleni na Pete ni marufuku kwa wanafunzi wetu wawapo shuleni au likizo. Pia ni marufuku wasichana kuvaa suruali, kaptula, nguo fupi au zinazobana uwapo shuleni au likizo.**

***Wavulana:***

- Njoo na suruali 2 Dark Blue zenye marinda mawili yenye mifuko 2 (miwili) pembeni, nyuma mfuko (1) mmoja upande wa kulia. Isiwe na turnup size (16-17)
- Njoo na mkanda mweusi
- Shati 2 mikono mifupi
- Tai 2 nyeusi
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye kamba na visigino vifupi (sio buti)
- Soksi nyeupe jozi mbili (2).
- Nguo za baridi atapewa sweta maalumu lenye nembo ya shule (la kijani) akifika shuleni.
- Truck suti ya Green (kijani) kwaajili ya michezo
- Viatu vya wazi vyeusi (open shoes) pair moja. Huvaliwa baada ya saa za madarasa **(siyo yeboyebo)**.
- Suti nyeusi kwa ajili ya uniform ya kanisani suruwali yenye marinda mawili yenye mifuko 2 (miwili)pembeni, nyuma mfuko (1) upande wa kulia koti lenye mikono mirefu lenye vishikizo viwili hadi vitatu na liwe na kola.
- Shati la light blue lenye mikono mirefu kuvalia suti siku ya ibada (Jumamosi) tu.
- Fulana za kuvalia ndani 2 nyeupe.
- Kanda mbili za bafuni

- Mwanafunzi atapewa sweta, 1, T-shirt 2, Kitabu cha nyimbo, Biblia ya Kiingereza, Lesson na Skafu vimelipiwa katika Ada.

**NB:** Mitindo ya kihuni ya nywele. Kunyoa kipara au panki, mavazi ya kihuni au yenye maandishi mabaya ni marufuku unapokuwa shuleni au likizo. Njoo na sare za shule tu. ***NGUO ZA NYUMBANI NI MARUFUKU*** **kwa wasichana na Wavulana.**

## 1. MAHITAJI YA BWENINI

Tafadhali njoo na vifaa vifuatavyo au waweza kuvipata shuleni kwa bei zilizoainishwa hapo chini:-

- ❖ Kikombe 500/=
- ❖ Sahani 1,500/=
- ❖ Kijiko 500/=
- ❖ Tochi 1 2,000/=
- ❖ Chandarua 10,000/=
- ❖ Blanketi 1 10,000/=
- ❖ Shuka **2 (Rangi ya Blue na Pink)** 16,000/=
- ❖ Godoro 2 ½ X 6 60,000/=
- ❖ Toilet papers 6 kila muhula(1@500/=) 3,000/=
- ❖ Galoni ya maji ya kunywa lita 5 2,000/=
- ❖ Ndoo ya plastiki 1 lita 10 au 20 3,500/=
- ❖ Soksi ndefu (stocking) 2,000/=
- ❖ Soksi fupi 1,000/=
- ❖ Tai nyeusi 1,500/=

## 2. KWA AJILI YA MASOMO AJE NA VITU HIVI.

. Madaftari makubwa (Counter books) 15 @ 2,500/=
. Mathematical set. 2,500/=
. Faili 1 (Spring file) 2,000/=
. Graph pad 02 @ 2,500/=
. Penseli na kifutio @ 1,00/=
. Rula 1- 500
. Kalamu za wino 5 au zaidi @ 2,00/=
. Kamusi ya Kiingereza na ya Kiswahili (Ni lazima)
. Sanduku la mbao au chuma lenye kufuli 1(Sanduku lisiwe la bati)

- Uje na vitabu vya kidato husika kwa masomo ya Civics, Kiswahili, English, History, Geography, Basic Mathematics, Biology, Physics, Chemistry, Agriculture na au Computer studies.

## G. MAMBO YA KIROHO

Shule hii hutoa elimu ya kiroho sambamba na elimu ya dunia hii. Unapowasili tafadhali kwa kicho na unyenyekevu mtafute <u>Bwana Mungu</u> wako kwa moyo wako wote na roho yako yote na kwa akili zako zote. Ukaishi, ukatende na kunena kwa hekima wakati wote na mahali pote.

Shule hii inakukaribisha kujiunga na kwaya, chama cha vijana **(AY, AMBASADOR, na PF**) na program zote za kiroho. Usifiche wala kuogopa kutumia vipaji mbalimbali ambavyo Mungu amekujalia. Kwa watakaopenda kujiunga na vyama vya vijana wanaweza kuja na uniform ya chama husika.

## UNAPOWASILI SHULENI

1. Nenda hadi Jengo la Utawala ambapo utapata maelekezo toka kwa Mwalimu wa zamu au katika ubao wa matangazo.

2. Ingia ofisi ya mhazini wa shule kwa ajili ya malipo ya fedha zote ulizoweka Benki (Pay-slip).

3. Kisha ingia ofisi ya msajili uonyeshe mambo yafuatayo:
   i. Risiti ya malipo yote
   ii. Sare ya shule
   iii. Barua hii ya kukuita shuleni
   iv. Picha (Passport size) zako na za watu watatu watakao kuwa wanakutembelea hapa shuleni.
   V. Faili moja (Spring file) na Graph pad 2.
4. Makamu Mkuu wa shule atakupatia fomu ya usajili kisha utafuata utaratibu uliooneshwa katika fomu hiyo.Aidha atakupatia student Handbook

5. Shule hii ni ya Kikristo. Iwapo utaonewa, kunyanyaswa, au kutendewa vyovyote kinyume na haki za kibinadamu tafadhali toa taarifa haraka kwa mkuu wa shule, Mwalimu au mlezi yeyote aliye karibu na eneo la tukio. Usijali hata kama ni usiku wa manane.

Mungu akubariki unapojiandaa na kusafiri kuja katika kituo hiki kizuri cha malezi ya kiakili, kiroho, kimwili na kijamii.

NB: Mawasiliano na shule kwa njia ya simu

| | |
|---|---|
| Mkuu wa Shule | 0784-288440 / 0621-267074/0765-434991 |
| Makamu Mkuu wa Shule | 0765-279024 |
| Mhazini wa Shule | 0757-141119 |
| Matron | **0756- 663663** |
| Patron | **0752 -811691** |

1. MAELEKEZO ZAIDI

Shule hii ni ya kikristo chini ya uendeshaji wa kanisa la Waadventista Wasabato. Wanaojiunga na shule hii ni watu wa madhehebu yote kwa masharti kuwa;-

1. Watahudhuria Ibada zote zilizo katika ratiba ya shule bila kukosa na kwa kicho.
2. Watasoma somo la Biblia toka kidato cha kwanza hadi kidato cha sita bila kuliacha kwa sababu zozote.
3. Watapumzika siku nzima ya **SABATO TAKATIFU YA BWANA** kama Biblia inavyofundisha.
4. Mzazi na mwanafunzi wanapokubali kujiunga na shule hii; mwanafunzi azingatie mambo yafuatayo:-

a. Kuvaa mavazi ya adabu, maridadi, masafi na yasiyo ya gharama kubwa sana.
b. Kuacha kabisa kutumia lugha ya matusi au ya kashfa kwa wanafunzi wenzake au mfanyakazi.
c. **Kuacha kabisa kuvaa nguo fupi, chini ya kiuno (kata K) sketi zilizopasuliwa, kupaka rangi midomo na kucha pamoja na kutumia madawa ya kuchubua ngozi na kubadili nywele shuleni au nje ya shule (likizo)sket zisivaliwe chini ya kitovu.**
d. Kuwa mwaminifu katika mambo yote kwa wanafunzi wenzake, walimu, wazazi na jamii yote.
e. Kuacha kabisa kupiga picha za aibu, kuwa na picha za aibu, kuandika au kuandikiwa barua za mapenzi au mawasiliano ya mapenzi kwa ajili yake au mwenzake.
f. Kuacha kabisa kutumia kutunza au kugawa madawa ya kulevya aina zote na pombe aina zote.
g. Lazima kuvuka darasa kwa wastani uliowekwa na shule
h. Hakikisha umepima afya kabla ya kuripoti shuleni na kujaza katika fomu iliyoambatanishwa kwenye barua hii.
i. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza unategemewa kuongea lugha hiyo wakati wote la sivyo utaadhibiwa vikali.

Watakaokiuka maagizo haya **WATAACHISHWA MASOMO** mara moja bila **KUSITA**.
Iwapo utakubaliana na maadili hayo ya kiroho na sheria zilizoelezwa ikiwa ni pamoja na kukubaliana naushauri wa kitaluuma endapo hautafikisha wastani wa shule **(45%)** tafadhali weka sahihi yako hapa, chini.

JINA LA MZAZI/MLEZI : ____________________

Namba ya simu ____________________

SAHIHI YA MZAZI MLEZI : ____________________

TAREHE: ____________________

JINA LA MWANAFUNZI: ____________________

SAHIHI YA MWANAFUNZI: ____________________

TAREHE: ____________________

<u>ZIARA ZA MAFUNZO</u>

Katika shule yetu mara zingine hutokea ziara za mafunzo, ziara za kikanisa na shughuli mbalimbali zitakazo mhitaji mwanafunzi kusafiri, kama m[illegible]zo, kwaya, na ziara za mafunzo. Hivyo mtoto wako anatakiwa kushiriki na wenzake ziara za ain[illegible]

Asante

.......................

*Joshua S. Okello*

MKUU WA SHULE

IKIZU SECONDARY SCHOOL HEAD OF SCHOOL P.O. Box 245 MUSOMA

KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO-JIMBO LA MARA
SHULE YA SEKONDARI IKIZU
S.L.P 245, MUSOMA-TANZANIA

MKATABA WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKIZU.

A. Huu ni mkataba wa kumsomesha mtoto hapa Ikizu Sekondari unaofanywa kati ya

SHULE YA SEKONDARI IKIZU na Ndugu_________________________________ambaye

ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi_________________________________________ambaye

amepata nafasi ya kusoma hapa Ikizu Sekondari katika kidato cha___________________

B. Masharti ya shule

Yafuatayo ni masharti ya shule ambayo mzazi/mlezi inambidi ayaelewe na ayaridhie kabla mtoto hajapokelewa shuleni.

1. Karo na michango yoyote ikishalipwa na mtoto akaamua kuhama au kuacha shule **haitarudishwa.**
2. Karo na michango ikishalipwa haitabadilishwa kutoka kwa mtoto mmoja hadi mwingine.
3. Kupiga au kupigana ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule.
4. Kumgomea mwalimu au mfanyakazi wa shule ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
5. Ulevi wa pombe, uvutaji sigara au madawa ya kulevya ni mwiko hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
6. Wizi wowote ama uharibifu wa mali ya shule wa makusudi ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
7. Uasherati ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
8. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule ni kosa kubwa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule.
9. Kwenda kwenye miji ya watumishi bila ruhusa ni marufuku.
10. Kukwepa masomo au mitihani na kutohudhuria vipindi bila ruhusa ya mwalimu wa somo au wa zamu ni kosa kubwa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
11. Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni ni marufuku na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
12. Kudharau, kukwepa au kukashifu ibada zinazoendeshwa shuleni ni kosa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
13. Kumiliki simu, radio, camera na vitu vyote vya aina hiyo ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule. Aidha vikikamatwa havitarudishwa kwa mtoto.
14. Wastani wa ufaulu wa wanafunzi mwisho wa mwaka kutoka kidato hadi kidato ni 45%. Mwanafunzi asiyefikia wastani atatakiwa kukariri kidato au kuhamia shule nyingine.
15. Tarehe ya kufika shuleni ni tarehe ya kufungua shule. Kila mwanafunzi afike shuleni siku hiyo.
16. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza. Kila mwanafunzi ajitahidi kuongea lugha hiyo ili kukwepa adhabu inayoweza kutolewa kwake akiongea lugha isiyorasmi.
17. Ni marufuku kudharau alama za Taifa letu. Mfano; wimbo wa taifa, fedha n.k

C. Tamko la Mzazi

Mimi ____________________________________________________

Mzazi/Mlezi wa ____________________________________________

nimeyasoma masharti ya shule na ninakubaliana nayo.

Sahihi ya mzazi/mlezi:__________________Tarehe:________________

**NB: Fomu hii ni lazima ikabidhiwe kwa Makamu Mkuu wa shule kabla ya usajili wa mtoto shuleni.**

**IKIZU HIGH SCHOOL**
**P.O. BOX 245, MUSOMA**

Name of Student ________________________________ sex (M/F__ Age____

**RE MEDICAL EXAMINATION**

The subject above refers.

Please, before reporting to school go to Regional or District Hospital for the diagnosis of the following diseases/healthy problems:-

1. Typhoid ______________________________________________________
2. Asthma _______________________________________________________
3. Tuberculosis (TB) ______________________________________________
4. HIV/AIDS ____________________________________________________
5. Yellow fever __________________________________________________
6. Sickle –cell ___________________________________________________
7. Any physical disability (eyes, etc)_________________________________
8. ______________________________________________________________
9. ______________________________________________________________
10. ______________________________________________________________
11. ______________________________________________________________
12. ______________________________________________________________

__________________________________________ ____________

Doctor's Name, Signature, Stamp Date